



NISHATI

HABARI ZA
NISHATI

News *Bulletin*

www.nishati.go.tz [Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara ya Nishati) [wizara_ya_nishati_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania) [@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017) [Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara ya Nishati)

Toleo Namba 19

Oktoba 1-31, 2020

KUMEKUCHA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA

Tanzania,
Uganda wasaini
makubaliano

JPM asema utekelezwaji
wake ni ushindi kwa
Watanzania na Waganda

Museveni aeleza
kufurahishwa na
hatua iliyofikiwa

Kalemani
abainisha Tanzania
itapata trilioni 7.5



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli na Rais wa Jamhuri ya Uganda, Yoweri Kaguta Museveni wakishuhudia Mawaziri wa Nishati wa nchi zao, Mary Goretti Kitutu wa Uganda (kushoto) na Dkt. Medard Kalemani wa Tanzania (kulia) wakitia saina Mkataba wa kuanza haraka Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) kwenye sherehe fupi iliyofanyika Uwanja wa Ndege wa Chato mkoani Geita Jumapili Septemba 13, 2020.

UK.
2

WAZIRI KALEMANI AZINDUA REA KITONGOJI KWA KITONGOJI

UK.
5



LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma

KUMEKUCHA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA

Na Mwandishi Maalum - Chato

Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, na Rais wa Jamhuri ya Uganda, Yoweri Kaguta Museveni, Septemba 13, 2020, walishuhudia utiaji saini wa makubaliano ya kukamilisha majadiliano ya utekelezaji wa mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi bandari ya Tanga nchini Tanzania.

Utiaji saini huo ulifanyika katika Uwanja wa Ndege wa Chato Mkoani Geita ambapo Waheshimiwa Marais hao pia walitia saini waraka wa pamoja wa kuagiza kuanza haraka kwa utekelezaji huo.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Tanzania na Uganda wakiwemo Mawaziri, Wanasheria Wakuu wa Serikali, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, viongozi na wataalamu wa Taasisi



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli akiongea mbele ya mgeni wake Rais wa Jamhuri ya Uganda, Yoweri Kaguta Museveni, mara baada ya kutia saini Waraka wa Pamoja unaoagiza kuanza haraka Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) kwenye sherehe fupi iliyofanyika Uwanja wa Ndege wa Chato, mkoani Geita, Septemba 13, 2020.

mbalimbali za Serikali na viongozi wa Vyama vya Siasa.

Akizungumza katika hafla hiyo, Rais Magufuli alimpongeza na kumshukuru Rais Museveni kwa kuchukua hatua madhubuti za kutafuta mafuta nchini mwake, na kukubali bomba lipitishwe nchini Tanzania.

Pia, Rais Magufuli

aliridhia asilimia 60 ya faida ichukuliwe na Tanzania ambapo bomba hilo linapita kwa zaidi ya asilimia 70 ilihali Uganda ikichukua faida kwa asilimia 40.

Rais Magufuli alisema kuwa kutekelezwa kwa mradi huo ni ushindi mkubwa wa kiuchumi kwa Uganda na Tanzania pamoja na Ukanda wa Afrika Mashariki na kuahidi

kuwa Tanzania itasimamia masuala yote yaliyobaki ili utekelezaji uanze haraka kwa manufaa ya Watanzania na Waganda.

Aidha, Rais Magufuli alieleza kuwa kutekelezwa kwa mradi huo kutarahisisha upelekaji wa gesi ya Tanzania nchini Uganda kupitia njia hiyo

INAENDELEA UK.

4



Rais wa Jamhuri ya Uganda Yoweri Kaguta Museveni akiongea baada ya kutia saini Waraka wa Pamoja unaoagiza kuanza haraka Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania), kwenye sherehe fupi iliyofanyika Uwanja wa Ndege wa Chato mkoani Geita Septemba 13, 2020



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli akimsindikiza Rais wa Jamhuri ya Uganda Yoweri Kaguta Museveni aliyekuwa akiwaaga Mawaziri wa Tanzania wakati akiondoka kurejea nyumbani baada ya kutia saini Waraka wa Pamoja unaoagiza kuanza haraka Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) kwenye sherehe fupi iliyofanyika Uwanja wa Ndege wa Chato mkoani Geita, Septemba 13, 2020.



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Mhandisi Zena Said
(Katibu Mkuu)

Makamu Mwenyekiti

Mhandisi Leonard Masanja
(Naibu Katibu Mkuu)

Mhariri

Veronica Simba

(Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini)

Waandishi

Veronica Simba
Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar

Msanifu Kurasa

Lucas Gordon

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano
Mtumba Dodoma, S.L.P.
2494, Dodoma

www.nishati.go.tz

[Wizara ya Nishati](#)

[@Nishati2017](#)

[wizara_ya_nishati_tanzania](#)

[Wizara ya Nishati](#)

UTEKELEZAJI MRADI WA BOMBA LA MAFUTA NI USHINDI KWETU SOTE

Septemba 13 mwaka huu, Marais Dkt. John Pombe Magufuli (Tanzania) na Yoweri Kaguta Museveni (Uganda), walishuhudia utiaji saine wa makubaliano ya kukamilisha majadiliano ya utekelezaji wa mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Bandari ya Tanga, nchini Tanzania.

Hii ni hatua kubwa na muhimu sana katika utekelezaji wa Mradi huo mkubwa utakaoleta manufaa kwa nchi yetu.

Imeelezwa kuwa kazi zilizokamilika hadi sasa ni pamoja na tafiti mbalimbali za kijiolojia, kijiofizikia na kijioteknikia pamoja na kukamilika kwa kazi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

Aidha, utwaaji wa ardhi katika maeneo ya miundombinu wezeshi upo katika hatua za mwisho za kukamilika. Kwa sasa kazi inayoendelea ni majadiliano ya mikataba mbalimbali kati ya nchi hodhi na wawekezaji wa Mradi huu.

Kama alivyosema Mheshimiwa

Rais Magufuli, kutekelezwa kwa Mradi huo ni ushindi mkubwa wa kiuchumi kwa Tanzania, Uganda na Ukanda wa Afrika Mashariki.

Miongoni mwa faida za Mradi ni ajira kwa Watanzania pamoja na fursa za biashara mbalimbali katika maeneo ambako bomba linapita.

Pia, kama ilivyobainishwa, Mradi ukikamilika utarahisisha upelekaji wa gesi ya Tanzania nchini Uganda sambamba na kurahisisha usafirishaji wa mafuta yanayotafutwa katika mbuga ya Wembele hapa nchini.

Hatuna budi kuipongeza Serikali yetu kwa kuridhia kutekeleza Mradi huo muhimu ambao ni mojawapo ya miradi mikubwa katika sekta ya nishati.

Aidha, tunapongeza jitihada za makusudi ambazo Serikali inafanya katika kuhakikisha Mradi unatekelezwa kwa ufanisi.

Tunatoa rai kwa wananchi kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali kwa kuchangamkia fursa mbalimbali zinazotokana na utekelezwaji wa Mradi huo.

Katunika Ki-nishati



KUMEKUCHA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli na Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wakipunga mikono kumuaga Rais wa Jamhuri ya Uganda Yoweri Kaguta Museveni, wakati akiiondoka kurejea nyumbani baada ya kutia saini Waraka wa Pamoja unaoagiza kuanza haraka Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) kwenye sherehe fupi iliyofanyika Uwanja wa Ndege wa Chato mkoani Geita, Septemba 13, 2020



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli akiongea jambo na Maafisa wa Uganda baada ya Rais wa Jamhuri ya Uganda Yoweri Kaguta Museveni kuondoka kurejea nyumbani baada ya kutia saini Waraka wa Pamoja unaoagiza kuanza haraka Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) kwenye sherehe fupi iliyofanyika Uwanja wa Ndege wa Chato, mkoani Geita, Septemba 13, 2020.

INATOKA UK.

2

hiyo na pia kutarahisisha usafirishaji wa mafuta yanayotafutwa katika mbuga ya Wembele nchini Tanzania.

Kwa upande wake, Rais Museveni alieleza kufurahishwa kwake na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huo na alibainisha kuwa kwa sasa jambo muhimu ni kuanza utekelezaji wa mradi ili wananchi waanze kuona

manufaa yake badala ya kupoteza muda mwingi zaidi katika majadiliano.

Rais Museveni alisema utafiti uliofanywa katika asilimia 40 ya bonde la mto Albert huko Hoima nchini Uganda umebaini kuwepo kwa mapipa bilioni 6.5 ya mafuta ghafi na kwamba zipo dalili njema kuwa asilimia 60 za eneo ambalo halijatafitiwa pia kuna mafuta na kwamba Uganda inatarajia kupata mafuta mengine katika ukanda wa Kadamu.

Alieleza kuwa, baada ya

kubaini kuwa waatalamu wa mataifa ya nje walikuwa wakimiyumbisha katika mpango wake wa kupata mafuta nchini Uganda, aliamua kuchukua hatua za kuwasomesha vijana wa Uganda.

Vijana hao walifanya utafiti na kisha kupata mafuta ambayo leo yamefikia hatua ya kuchimbwa. Alitoa wito kwa wananchi wa Tanzania na Uganda kuamka na kuchapa kazi za uzalishaji mali kwa maendeleo.

Naye Waziri wa

Nishati, Dkt. Medard Kalemuni alisema bomba litakalojengwa litakuwa na urefu wa kilometa 1,445 ambapo kilometa 1,149 kati yake zinapita nchini Tanzania.

Aidha, alisema bomba litapita katika mikoa 8, wilaya 24 na vijiji 280 hapa nchini. Alieleza zaidi kuwa, litakuwa na uwezo wa kupitisha mapipa 216,000 kwa siku, litazalisha ajira 10,000 na kwamba kwa miaka 25 ya Mradi huo, Tanzania itapata mapato ya shilingi trilioni 7.5.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli akimlaki mgeni wake Rais wa Jamhuri ya Uganda Yoweri Kaguta Museveni, alipowasili kutia saini Waraka wa Pamoja unaoagiza kuanza haraka Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania). Utiaji saini huo ulifanyika wakati wa sherehe fupi katika Uwanja wa Ndege wa Chato mkoani Geita, Septemba 13, 2020.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli na Rais wa Jamhuri ya Uganda Mhe. Yoweri Kaguta Museveni, wakitia saini Waraka wa Pamoja unaoagiza kuanza haraka Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania), wakati wa sherehe fupi iliyofanyika Uwanja wa Ndege wa Chato, mkoani Geita, Septemba 13, 2020.

WAZIRI KALEMANI AZINDUA REA KITONGOJI KWA KITONGOJI



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa Kitongoji cha Migombani, Kijiji cha Bukene, Wilaya ya Nzega, mkoani Tabora (hawapo pichani), wakati wa uzinduzi wa mradi wa umeme kwa kila kitongoji nchini uliofanyika Septemba 24, 2020, mkoani humo.

Zuena Msuya na Hafsa Omar - Tabora

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani amezindua rasmi usambazaji wa umeme katika kila kitongoji nchini ambapo jumla ya vitongoji 64,839 nchini kote vinatarajiwa kuunganishwa na nishati



Wananchi wa Kitongoji cha Migombani, Kijiji cha Bukene, Wilaya ya Nzega, mkoani Tabora, wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani), wakati wa uzinduzi wa mradi wa umeme kwa kila kitongoji nchini uliofanyika Septemba 24, 2020, mkoani humo.

hiyo kwa kipindi cha miezi 12 kuanzia sasa.

Uzinduzi huo ulifanyika katika Kitongoji na Kijiji cha Ufuruma, wilayani Uyui na katika Kitongoji cha Migombani, Kijiji cha Bukene wilayani Nzega, Mkoa wa Tabora, Septemba 24, 2020.

Akizungumza na wananchi katika hafla hiyo, Dkt. Kalemani alisema kuwa mradi huo utagharimu fedha za kitanzania shilingi bilioni 297.7 na kwamba utakuwa endelevu.

Alibainisha sababu ya kuichagua Tabora kuwa kitovu cha kuzindua mradi huo, kwamba ni Mkoa mkubwa ikilinganishwa na mikoa mingine nchini, pia una idadi kubwa ya vitongoji ambavyo bado havijaunganishwa kabisa na umeme.

Katika mkoa huo, vitongoji 122 vinatarajiwa kuunganishwa umeme na kampuni ya ukandarasi ya Sengerema ambayo imeahidi kutekeleza kazi hiyo ndani ya kipindi cha miezi tisa, badala ya 12

iliyoainishwa kimkataba. "Naomba tuelewane Watanzania, Rais Magufuli alikwishatoa fedha za kupeleka umeme kwenye vijiji vyote na vitongoji vyote. Niwaombe wananchi, kwenye masuala ya umeme tulieni, umeme unakuja kila kitongoji. Sasa ni rasmi kuwa vitongoji vyote vinaletewa umeme, mnachotakiwa wananchi ni kusuka nyaya katika nyumba zenu maana umeme huu haubagui nyumba," alisisitiza Dkt. Kalemani.

Aidha, aliwataka wananchi kuendelea kulipia gharama za kuunganishiwa umeme bila kusubiri nguzo kuwafikia kwa kuwa tayari umeme utafika katika kila kitongoji kwa gharama ya shilingi 27,000 tu.

Alisema kuwa wananchi hawapaswi kuhoji kuhusu nguzo kufika katika maeneo yao kwakuwa hilo siyo jukumu lao bali wanachotakiwa kufanya ni kulipia gharama za kuwashwa umeme tu, na

INAENDELEA UK.

6



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, akikata utepe kuashiria uzinduzi wa usambazaji umeme katika kila kitongoji nchini, uliofanyika katika Kitongoji cha Migombani, Kijiji cha Bukene, Wilaya ya Nzega, mkoani Tabora, Septemba 24, 2020. Kushoto kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dkt. Philemon Sengati na kulia kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Wakili Julius Kalolo.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akiweka jiwe la msingi la usambazaji umeme katika kila kitongoji nchini, uliofanyika katika Kitongoji cha Migombani, Kijiji cha Bukene, Wilaya ya Nzega, mkoani Tabora, Septemba 24, 2020.

WAZIRI KALEMANI AZINDUA REA KITONGOJI KWA KITONGOJI



Jiwe la msingi wa mradi wa usambazaji umeme kwa kila kitongoji nchini lililowekwa na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani wakati wa hafla ya uzinduzi rasmi wa mradi huo uliofanyika katika Kitongoji cha Migombani, Kijiji cha Bukene, Wilaya ya Nzega, mkoani Tabora, Septemba 24, 2020.

INATOKA UK.

5

baada ya kulipia gharama ndipo wahoji endapo hawajawashiwa umeme.

Aliitaka Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kushirikiana na serikali za vijiji, wilaya na mkoa kutoa elimu na kuwahamasisha wananchi juu ya umuhimu wa umeme.

Hata hivyo aliwaonya baadhi ya wakandarasi wenye tabia ya kuruka nyumba za wateja kuwa hiyo haitakubalika na yeyote atakayebainika kufanya hivyo,

atachukuliwa hatua za kisheria.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa huo, Dkt. Philemon Sengati aliwaasa wananchi kuchangamkia fursa ya umeme kwa kuanzisha viwanda vidogo ili kuinua uchumi wao na Taifa kwa jumla.

Aidha, aliwataka kutunza miundombinu ya mradi huo na kutoa ushirikiano kwa wakandarasi wanaotekeleza. Pia, aliwaasa vijana watakaopata ajira kuwa wazalendo huku wakizingatia kuwa miradi hiyo ni kwa ajili ya Watanzania.



Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma, akiwasalimia wananchi wa Kitongaji cha Ufuruma, Kijiji cha Ufuruma, Wilaya ya Uyu, Mkoa wa Tabora, wakati wa hafla ya uzinduzi wa mradi wa usambazaji umeme kwa kila kitongoji nchini, uliofanyika Septemba 24, 2020. Kulia ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu kutoka Wizara ya Nishati, Raphael Nombo.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (mwenye shati la bluu) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Tabora pamoja na viongozi kutoka Wizara ya Nishati, mara baada ya uzinduzi rasmi wa mradi wa usambazaji umeme kwa kila kitongoji nchini, uliofanyika katika Kitongaji cha Ufuruma, Kijiji cha Ufuruma, Wilaya ya Uyu, mkoani Tabora, Septemba 24, 2020.

Viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake, wakifurahia uzinduzi wa mradi wa usambazaji wa umeme katika kila kitongoji nchini, uliofanyika katika Kitongaji cha Ufuruma, Kijiji cha Ufuruma, Wilaya ya Uyu, mkoani Tabora.

MRADI WA UMEME JULIUS NYERERE KUKAMILIKA KWA WAKATI

Hafsa Omar - Pwani

Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani, amesema ujenzi wa Mradi mkubwa wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP) utakamilika kwa wakati na kwa kiwango cha kimataifa.

Aliyasema hayo, Septemba 6, 2020, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi huo unaotekelezwa kwenye mto Rufiji.



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (kushoto) na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said wakiwa kwenye kikao pamoja na wataalamu mbalimbali kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) (hawapo pichani), kabla ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Mradi wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP), Septemba 6, 2020.



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (mwenye shati la bluu) na Naibu Waziri wa Ujenzi wa Misri, Jenerali Mahmoud Nassar (mwenye suti) wakiwa na wataalamu mbalimbali kutoka Tanzania na Misri wakiangalia picha za Mradi mkubwa wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP), Septemba 6, 2020. Viongozi hao walikagua maendeleo ya ujenzi wa Mradi huo.

Katika ziara hiyo, Waziri aliambatana na Naibu Waziri wa Ujenzi wa Misri, Jenerali Mahmoud Nassar, Katiku Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said na Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Edward Ishengoma.

Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Dkt Alexander Kyaruzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo, Dkt Tito Mwinuka na wataalamu mbalimbali kutoka Tanzania na Misri.

Waziri alieleza kuwa tayari Serikali imemlipa mkandarasi wa mradi huo zaidi ya shilingi trilion 1.49, ambayo ni sawa na asilimia 100 ya malipo ambayo alitakiwa kulipwa hadi sasa.

“Tunataka mradi ukamilike kwa wakati na kwa kiwango cha juu. Siyo mradi unakamilika baada ya miezi miwili unaanza kuhitaji tena ukarabati kwa gharama nyingine, kwa hili hatutakubali. Hivyo, nitoe wito kwa mkandarasi kufanya kazi kwa weledi na kiwango cha juu,” alisisitiza.

Alisema kuwa, Serikali imekuwa ikifuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa mradi huo, ili kuhakikisha unakamilika ndani ya muda uliopangwa.

Katika juhudi za kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati, Dkt. Kalemani alitoa maagizo kwa Mkandarasi kuhakikisha kuwa ifikapo mwisho wa mwezi Septemba 2020, awe amekamilisha kazi ya ujenzi wa handaki ambao ameelezea kuwa muhimu na unaotegemewa kwa kiasi kikubwa kuendesha mradi husika.



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akizungumza kwenye kikao baina ya Ujumbe kutoka Serikali ya Tanzania na Misri, kabla ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Mradi mkubwa wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP), Septemba 6, 2020. Kushoto ni Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said na kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Dkt Alexander Kyaruzi.

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (kulia) na Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma, wakiwa katika kikao baina ya Ujumbe kutoka Serikali ya Tanzania na Misri kabla ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Mradi mkubwa wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP), Septemba 6, 2020.

Naibu Waziri wa Ujenzi wa Misri, Jenerali Mahmoud Nassar akizungumza na Waandishi wa Habari mara baada ya kumaliza kukagua maendeleo ya ujenzi wa Mradi mkubwa wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP), Septemba 6, 2020. Kushoto kwake ni Waziri wa Nishati (Tanzania), Dkt Medard Kalemani.

INATOKA UK.

7

MRADI WA UMEME JULIUS NYERERE KUKAMILIKA KWA WAKATI

Vilevile, alimtaka Mkandarasi huyo kuhakikisha anaajiri waatalamu wote ambao wanahitajika katika ujenzi wa mradi huo na ifikapo mwisho wa mwezi Septemba wawe tayari wamefika nchini kwa ajili ya ujenzi huo.

“Hatuna wasiwasi na ajira zinazotolewa hapa kwenye mradi. Hadi sasa umeajiri zaidi ya Watanzania 4,500 na kwa wale waliobaki natoa wito waajiriwe ili kazi ziweze kwenda kwa haraka,” alisema Dkt Kalemani.

Pia, aliangaza

uharakishwaji wa ujenzi wa nyumba za wafanyakazi ili wahamie katika eneo hilo na kuwawezesha kufanya kazi zao kwa muda mrefu ili mradi huo uweze kukamilika mapema.

Dkt Kalemani, alisema kuwa mradi huo ndiyo utakaotatua matatizo yote ya umeme nchini na kuahidi kuwa Serikali itasimamia kikamilifu ujenzi wake ambao utasaidia pia usambazaji

wa umeme kwenye vijiji na vitongoji nchini.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Ujenzi wa Misri, Jenerali Mahmoud Nassar, alisema kuwa, Rais wa nchi yao anafuatilia kwa karibu utekelezaji wa mradi huo na ameahidi kuhakikisha kuwa unakamilika kwa wakati.

Aidha, alisema kuwa mradi huo utakamilika kwa mafanikio makubwa kwa sababu ya ushirikiano

mkubwa wanaopata kutoka kwa Watanzania. Aidha, alieleza kuwa mradi huo utakapokamilika utaleta maendeleo makubwa nchini.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said alisema maendeleo ya mradi huo ni mazuri. Aliwataka Watanzania kuendelea kuunga mkono mradi huo wenye faida nyingi kwa Taifa.



Ujumbe kutoka Serikali ya Tanzania ukiongozwa na Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani na Ujumbe kutoka Misri ukiongozwa na Naibu Waziri wa Ujenzi wa Misri, Jenerali Mahmoud Nassar, wakikagua maendeleo ya ujenzi wa Mradi mkubwa wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP), Septemba 6, 2020.

MRADI WA UMEME RUSUMO UNA MANUFAA MTAMBUKA KWA WATANZANIA - SERIKALI



Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Luteni Kanali Michael Mtenjele (kushoto), akizungumza na Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo kabla ya kuanza ziara ya kazi yenye lengo la kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa kupitia Mradi husika, Septemba 28, 2020.

Veronica Simba – Ngara

Serikali imeeleza kuwa Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera, unaotekelezwa Rusumo wilayani Ngara, una manufaa mtambuka kwa Watanzania.

Hayo yalielezwa, Septemba 28, 2020 na Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi huo ikihusisha Wakurugenzi wa Bodi na Kamati ya Ufundi, wakiwa katika ziara ya kazi yenye lengo la kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa kupitia Mradi husika.

Akizungumza baada ya ziara hiyo, Kiongozi wa Timu hiyo, Mhandisi Innocent Luoga ambaye ni Mjumbe wa Bodi wa Kamati husika, alisema mbali na umeme, Mradi huo utawanufaisha Watanzania kupitia miradi mbalimbali ya kijamii ambayo alisema iko katika hatua nzuri za

utekelezaji.

Mhandisi Luoga ambaye pia ni Kamishna Msaidizi wa Umeme kutoka Wizara ya Nishati alieleza kuwa miradi ya kijamii inayotekelezwa ni pamoja na inayohusu sekta za afya, elimu, maji, mifugo na kilimo.

Akizungumzia lengo la Timu hiyo ya Serikali kutembelea miradi ya kijamii inayoendelea kutekelezwa, Mhandisi Luoga alisema ni kujionea hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wake, kubaini changamoto zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi ili kuwezesha miradi hiyo kukamilika kwa wakati.

“Tumetembelea shule za msingi na sekondari, zahanati, vituo vya afya na miradi ya maji ambayo yote inayotekelezwa hapa Ngara na tumejiridhisha kuwa kwa sehemu kubwa imefika hatua nzuri na baadhi yake imekamilika.”

Hata hivyo, alieleza kuwa Timu yake imebaini changamoto ya baadhi

ya miradi kusuasua hususan Mradi wa Maji unaotekelezwa Rusumo ambao umechelewa kutokana na kukosekana vibali vya ujenzi.

Alisema yeyé na wenzake wametatu changamoto husika kwa kuelekeza vibali hivyo vipatikane haraka ili Mkandarasi aanze kazi na kukamilisha Mradi kwa wakati.

Aidha, kwa miradi mingine inayokusua inayohusu majengo ya shule na vituo vya afya, Timu iliwataka wakandarasi husika kukamilisha kazi kwa wakati, kuzingatia viwango na ubora.

Kuhusu manufaa ya umeme, Mhandisi Luoga alieleza kuwa Mradi wa Rusumo utakapokamilika utazalisha megawati 80 ambazo zitagawanywa kwa nchi tatu zinazohusika ambazo ni Tanzania, Rwanda na Burundi kwa kila moja kupata megawati 27.

Alisema kuwa kwa upande wa Tanzania, Mradi utasaidia kuongeza umeme katika gridi ya Taifa pamoja na kuboresha hali ya upatikanaji nishati hiyo katika Mkoa wa Kagera.

“Kama alivyoelekeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt John Pombe Magufuli, kuwa Mkoa wa Kagera uingizwe katika gridi ya Taifa, hivyo kukamilika kwa Mradi wa Rusumo kutawezesha hilo.”

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Luteni Kanali Michael Mtenjele, akizungumza na Timu hiyo ofisini kwake kabla ya kuanza ziara, alipongeza kazi nzuri inayoendelea kufanyika ambayo alisema imeleta manufaa makubwa kwa wananchi wake.

“Miundombinu ambayo imejengwa ni ya kipekee. Hatukuzoea kuona Shule za Msingi zinakuwa na Jengo la Utawala lakini kupitia Mradi huu hilo limefanyika na kwakweli inapendeza sana,” alifafanua.

Naye Mratibu wa Miradi ya Maendeleo ngazi ya Wilaya, Herman Hume alieleza kuwa miradi hiyo ya kijamii inayoendelea kutekelezwa wilayani Ngara ilitengewa fedha kiasi cha dola milioni tano za Marekani ambazo ni sawa na takribani shilingi bilioni 12 za Tanzania.

Wengine wanaoshiriki katika ziara hiyo itakayoendelea kwa siku mbili nyingine ni Mhandisi Salum Inegeja kutoka Wizara ya Nishati na Mhandisi Costa Rubagumya kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Ufundi ya Mradi wa Rusumo.

Pia, Timu imefuatana na Mhandisi Patrick Lwesya, Meneja Mradi wa Rusumo, Gaspar Mashingia, Afisa Mwandamizi, Jamii, Maendeleo na Uhamaji Makazi pamoja na Maaafisa kadhaa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.



Baadhi ya wanafunzi wakiwa katika foleni kuingia chumba cha Daktari katika Zahanati ya Kijiji cha Kyenda iliyoko wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera. Taswira hii ilichukuliwa Septemba 28, 2020 wakati wa ziara ya Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo (pichani), kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa na Mradi huo. Zahanati hii imejengwa kupitia Mradi husika.



Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo ikikagua tanki la maji linalojengwa katika Kitongoji cha Ngome, Kijiji cha Kasulo, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera kupitia Mradi huo, Septemba 28, 2020. Timu hiyo ilikuwa katika ziara kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa na Mradi huo.



Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo ikikagua nyumba ya kuishi walimu katika Shule ya Sekondari Mumiterama, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera iliyojengwa kupitia Mradi huo. Timu hiyo ilikuwa katika ziara kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa na Mradi huo Septemba 28, 2020.



Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo ikikagua ujenzi wa Tanki la Maji, eneo la Rusumo, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera. Timu hiyo ilikuwa katika ziara kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa na Mradi huo Septemba 28, 2020.



Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo ikikagua Jengo la Madarasa katika Shule ya Sekondari Mumiterama, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera iliyojengwa kupitia Mradi huo. Timu hiyo ilikuwa katika ziara kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa na Mradi huo Septemba 28, 2020.



Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo ikizungumza na wanafunzi wa darasa la pili katika Shule ya Msingi Rusumo iliyoko kijiji cha Kyenda, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera. Timu hiyo ilikuwa katika ziara kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa na Mradi huo Septemba 28, 2020 ambapo Shule hiyo imenufaika kwa kujengwa vyumba vya madarasa na vyoo vya wanafunzi.



Sehemu ya majengo ya Kituo cha Afya Rusumo, kilichoko wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera, kinachojengwa kupitia Mradi wa Umeme wa Rusumo unaotekelezwa wilayani humo. Taswira hii ilichukuliwa Septemba 28, 2020 wakati wa ziara ya Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi huo, kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa kupitia Mradi husika.



Baadhi ya wajumbe wa Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo wakijadiliana jambo nje ya Zahanati ya Kijiji cha Kyenda, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera baada ya kufanya ukaguzi katika Zahanati hiyo wakiwa katika ziara ya kazi, Septemba 28, 2020. Kutoka kulia ni Kiongozi wa Msafara, Mhandisi Innocent Luoga ambaye ni Kaimu Kamishna kutoka Wizara ya Nishati na Mjumbe wa Bodi ya Mradi huo, Mhandisi Salum Inegeja kutoka Wizara ya Nishati na Mhandisi Costa Rubagumya kutoka TANESCO ambao ni wajumbe wa Kamati ya Ufundi ya Mradi.



Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo wakijadiliana jambo baada ya kukagua vyoo vya wanafunzi katika Shule ya Sekondari Mumiterama, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera vilivyojengwa kupitia Mradi huo. Timu hiyo ilikuwa katika ziara kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa na Mradi huo Septemba 28, 2020.

MARUFUKU MKANDARASI KUPEWA KAZI ZAIIDI YA MKOA MMOJA - KALEMANI

**Hafsa Omari na
Zuena Msuya - Tabora**

Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani

amesema kuanzia sasa ni marufuku kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini, kupewa kazi katika mkoa zaidi ya mmoja na badala yake watapewa kwa kila wilaya bila kujali idadi ya vijiji vilivyopo.

Alisema hayo kwa nyakati tofauti, mkoani Tabora alipokuwa akizindua rasmi mradi wa usambazaji umeme kitongoji kwa kitongoji uliofanyika katika wilaya za Uyui na Nzega mkoani humo, Septemba 24, 2020 huku akibainisha kuwa mradi huo utavifika vitongoji vyote nchini.

Akieleza sababu za uamuzi huo wa kuwapatia wakandarasi husika kazi za wilaya, alisema ni kuhakikisha kuwa miradi hiyo inakamilika kwa haraka ndani ya muda mfupi na kwa wakati.

"Mathalani, mkandarasi anaweza kupewa wilaya



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (katikati) akisaini kitabu cha wageni alipowasili katika hafla ya uzinduzi wa usambazaji wa umeme kwa kila kitongoji nchini, uliofanyika katika Kitongoji na Kijiji cha Ufuruma, wilayani Uyui, Mkoa wa Tabora, Septemba 24, 2020. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dkt. Philemon Sengati na kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati vijijini (REA), Wakili Julius Kalolo.

moja yenye vijiji 20 au 70. Jukumu lake ni kumaliza kwa wakati ili kuondoa changamoto ya kutomaliza miradi kwa wakati."

Aliongeza kuwa, mkandarasi atakayechelewesha mradi atachukuliwa hatua za kimkataba, kisheria na za kiusimamizi kwakuwa maeneo ya utekelezaji wa miradi yamepunguzwa tofauti na ilivyokuwa awali.

Aidha, alisema kuwa hakutakuwa na muda wa nyongeza kwa yeyote atakayechelewesha mradi na badala yake atakatwa asilimia 10 ya fedha zake

kama adhabu na mradi huo atapewa mtu mwingine.

"Hatua hii itaondoa visingizio kwa baadhi ya wakandarasi wenye tabia hiyo ya kuchelewesha mradi. Wengine walikuwa wanasingizia ukubwa wa eneo, wengine miundombinu au vifaa havitoshi ama kutofika kwa wakati. Sasa, hii itamaliza sababu zote za kuchelewesha miradi,"

alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Dkt. Kalemani alilisisitiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuwakatia umeme wateja wenye madeni sugu ili ikupata fedha za kulijengea uwezo shirika hilo kutoa huduma bora na kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

"Endapo kuna Taasisi au Shirika la Umma linadaiwa ndani ya siku 14 msiwaoneee aibu, nendeni mkakate umeme, na wakiwapigia simu kuomba kurudishiwa msikubali, na mimi nikipigiwa sitaruhusu waunganishwe hadi pale watakapokuwa wamelipia," alisema Dkt. Kalemani.

Aliwaagiza Mameneja wa Kanda, Mikoa na Wilaya, kutowaonea huruma wateja wa namna hiyo kwa kuwa wanarudisha nyuma maendeleo ya shirika hilo na kusababisha wananchi wengine kukosa huduma bora kwa wakati.



Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa Kitongoji na Kijiji cha Ufuruma, Wilaya ya Uyui, mkoani Tabora, wakati wa hafla ya uzinduzi wa mradi wa usambazaji umeme kwa kila kitongoji nchini, uliofanyika Septemba 24, 2020.



Transfoma ikiwa imesimikwa katika kijiji cha Ufuruma, wilayani Uyui. na baadhi ya Kampuni za ukandarasi zinazotekeleza Mradi wa Usambazaji wa Umeme katika Vijiji mbalimbali nchi.

NGARA WASISITIZWA KUTUNZA MIRADI YA KIJAMII



Wajumbe wa Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo wakikagua miundombinu ya maji katika Shule ya Msingi Makugwa iliyopo katika kijiji cha Mukubu, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera wakiwa katika ziara ya kazi, Septemba 29, 2020. Shule hiyo ni mojawapo ya wanufaika wa miradi ya kijamii inayotekelezwa na Mradi husika ambapo imejengwa vyumba vya madarasa, Ofisi na nyumba za walimu, vyoo vya wanafunzi pamoja na tanki la maji safi. Kutoka kushoto ni Mhandisi Innocent Luoga, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mradi na Kiongozi wa Msafara, Herman Hume, Mratibu wa Miradi ya Maendeleo ngazi ya Wilaya na Mhandisi Costa Rubagumya ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Ufundi ya Mradi.

Veronica Simba – Ngara

Serikali imewaasa wananchi wa Ngara, Mkoa wa Kagera kutunza miradi mbalimbali ya maendeleo ya kijamii, inayoendelea kutekelezwa wilayani humo kupitia Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera (megawati 80).

Wito huo ulitolewa Septemba 29, 2020 na Timu

ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi huo ikihusisha Wakurugenzi wa Bodi na Kamati ya Ufundi, wakiwa katika ziara ya kazi yenye lengo la kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa kupitia Mradi husika.

Akizungumza kwa nyakati tofauti na Maafisa Watendaji pamoja na wananchi katika maeneo mbalimbali kulipo na miradi hiyo, Kiongozi wa Timu hiyo, Mhandisi



Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo ikikagua banda kitalu maarufu kama 'green house' kwa lugha ya kigeni lililoandaliwa kwa ajili ya kilimo cha kisasa katika kijiji cha Chivu, Kata ya Ntoreye, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera, Timu hiyo ilikuwa katika ziara kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa na Mradi huo, Septemba 29, 2020.

Innocent Luoga ambaye ni Mjumbe wa Bodi wa Kamati husika, alisema endapo miundombinu hiyo ya miradi husika isipotunzwa, itakuwa ni hasara kwa Serikali na wananchi walengwa.

"Miradi hii inayohusisha shule, vituo vya afya, miradi ya maji, miundombinu ya kilimo na ufugaji bora inalenga kuwanufaisha wananchi, hivyo ili lengo hilo litimie, inabidi itunzwe."

Timu hiyo ikiwa katika siku ya pili ya ziara yake, ilitembelea miradi kadhaa ikiwemo Shule ya Msingi Makugwa iliyopo katika

kijiji cha Mukubu ambayo imenufaika na Mradi huo kwa kujengwa vyumba vya madarasa, Ofisi na nyumba za walimu, vyoo vya wanafunzi pamoja na tanki la maji safi.

Mwalimu Siyajali Manyasi ambaye ni Mkuu wa Shule hiyo aliuweleza Ujumbe huo wa Serikali kuwa, kujengwa kwa miundombinu hiyo kumeiwezesha Shule hiyo kupata usajili na kujitegemea kutoka kuwa tawi la Shule ya Msingi

INAENDELEA UK.

13



Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo ikikagua mradi wa ufugaji nyuki katika kijiji cha Chivu, Kata ya Ntoreye, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera, Timu hiyo ilikuwa katika ziara kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa na Mradi huo, Septemba 29, 2020.



Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo ikikagua miundombinu mbalimbali ya karakana ya useremala na ushonaji nguo katika Chuo cha Ufundi Stadi Lemera kilichopo katika kijiji cha Mukibogoye, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera. Timu hiyo ilikuwa katika ziara kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa na Mradi huo, Septemba 29, 2020.

NGARA WASISITIZWA KUTUNZA MIRADI YA KIJAMII

INATOKA UK.

12

Mukubu iliyoko umbali mrefu kutoka hapo.

“Uwepo wa Shule hii umewapunguzia watoto adha ya kutembea mwendo mrefu takribani kilomita 10 kwenda Mukubu na pia uwepo wa majengo haya ya kisasa umevutia wazazi wengi zaidi kuwaleta watoto wao shuleni,” alisema Mwalimu Manyasi.

Vilevile, Timu hiyo ilitembelea Shule ya Sekondari Bukiriro ambayo imenufaika kwa kujengewa bweni la wanafunzi wa kike, bwalo la chakula na vyoo.

Aidha, Ujumbe huo ulitembelea Chuo cha Ufundi Stadi Lamera kilichopo katika kijiji cha Mukibogoye kilichonufaika kwa kujengewa karakana ya useremala na ushonaji nguo pamoja na uwanja wa michezo ambao ujenzi wake unaendelea.

Timu ilitembelea pia miradi ya kilimo cha kisasa kwa njia ya banda kitalu

maarufu kama ‘green house’ kwa lugha ya kigeni na mradi wa ufugaji nyuki, inayotekelezwa katika kijiji cha Chivu, Kata ya Ntobeye, yote ikilenga kuwanufaisha wananchi kiuchumi.

Akizungumza katika ziara hiyo, Mratibu wa Miradi wa Maendeleo ngazi ya Wilaya, Herman Hume alieleza kuwa miradi hiyo ya kijamii inayoendelea kutekelezwa wilayani Ngara ilitengewa fedha kiasi cha dola milioni tano za Marekani ambazo ni sawa na takribani shilingi bilioni 12 za Tanzania.

Kwa upande wao, Mhandisi Salum Inegeja kutoka Wizara ya Nishati na Mhandisi Costa Rubagumya kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Ufundi ya Mradi wa Rusumo, walikiri kurudhishwa na utekelezwaji wa miradi hiyo lakini wakasisitiza umuhimu wa kuifanya iwe endelevu kwa maslahi ya wananchi.

Katika ziara hiyo,



Mjumbe wa Kamati ya Ufundi ya Mradi wa Umeme wa Rusumo unaotekelezwa wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera, Mhandisi Salum Inegeja, akiwa amekaa katika Ofisi ya Walimu, Shule ya Msingi Makugwa iliyopo katika kijiji cha Mukubu, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera.

Timu ilifuatana pia na Mhandisi Patrick Lwesya, Meneja Mradi wa Rusumo, Gaspar Mashingia, Afisa Mwandamizi, Jamii, Maendeleo na Uhamaji Makazi pamoja na Maafisa kadhaa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.

Mradi wa Umeme Rusumo unatekelezwa kwa ushirikiano wa nchi tatu za Tanzania, Rwanda na Burundi ambapo utakapokamilika unatarajiwa kuzalisha megawati 80 za umeme zitakazogawanywa kwa nchi husika.



Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo ikizungumza na wanafunzi katika Shule ya Msingi Makugwa iliyopo katika kijiji cha Mukubu, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera. Timu hiyo ilikuwa katika ziara kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa na Mradi huo Septemba 29, 2020 ambapo Shule hiyo imenufaika kwa kujengewa vyumba vya madarasa, nyumba na ofisi za walimu, tanki la maji savi na vyoo vya wanafunzi.



Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mradi wa Umeme Rusumo ambaye pia ni Kamishna Msaidizi wa Umeme kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga (kulia), akimsisitiza Mwalimu Mkuu (kushoto) wa Shule ya Msingi Makugwa iliyopo katika kijiji cha Mukubu, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera, kutunza miundombinu iliyojengwa katika shule hiyo.



Bweni la wanafunzi wa Kike katika Shule ya Sekondari Bukiriro, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera, lililojengwa kupitia Mradi wa Umeme Rusumo. Taswira hii ilichukuliwa Septemba 29, 2020 wakati wa ziara ya Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi huo, kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa kupitia Mradi husika.



Mjumbe wa Kamati ya Ufundi ya Mradi wa Umeme wa Rusumo unaotekelezwa wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera, Mhandisi Costa Rubagumya (kushoto), akizungumza jambo wakati wa ziara ya Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi huo, Septemba 29, 2020. Hapa ni Shule ya Sekondari Bukiriro ambayo ni mnufaika wa Mradi huo. Kulia ni Mjumbe wa Bodi ya Mradi huo, Mhandisi Innocent Luoga na katikati ni Gaspar Mashingia, Afisa Mwandamizi, Jamii, Maendeleo na Uhamaji Makazi.



Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Robert Syantemi, akikata utepe kuashiria uwashwaji wa umeme katika kijiji cha Lendikinya wilayani Monduli, Septemba 11, 2020.



Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Robert Syantemi akiwa katika picha ya pamoja na Timu Maalum ya Serikali iliyoungwa na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani kufuatilia utekelezaji wa miradi ya umeme mijini na vijijini. Timu hiyo pamoja na mambo mengine ilifanikisha kuwashwa umeme katika kijiji cha Lendikinya wilayani Monduli, Septemba 11, 2020.

TIMU MAALUM YA SERIKALI YAWASHA UMEME LENDIKINYA

Na Mwandishi wetu - Arusha

Timu maalum ya Serikali iliyoungwa hivi karibuni na Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani, imewasha umeme katika kijiji cha Lendikinya, wilayani Monduli wakati ikiendelea na kazi ya kufuatilia utekelezaji wa miradi ya umeme mijini na vijijini, Septemba 11, 2020.

Akiwasha umeme katika Zahanati ya kijiji cha Lendikinya na katika baadhi ya makazi ya wananchi, Kamishna Msaidizi wa Umeme kutoka Wizara ya Nishati,

Mhandisi Innocent Luoga alisema utekelezaji wa Mradi huo ni kutokana na maagizo ya Waziri Kalemani.

“Waziri alifanya ziara katika kijiji hiki na kubaini kusuasua kwa Mkandarasi aliyekuwa akitekeleza Mradi huu, hivyo akamfukuza kazi na kuagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mkoa wa Arusha ikamilishe kazi husika.”

Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Wilaya ya Monduli ambaye alimwakilisha Mkuu wa Wilaya hiyo, Robert Syantemi, aliwataka wananchi kutumia fursa

zinazotokana na uwepo wa umeme katika kuzalisha mazao ya kilimo na mifugo na kuyaongezea thamani, pamoja na kubuni miradi mingine midogo midogo ili kujiongeza kipato.

Aidha alitaka TANESCO kuongeza utoaji wa huduma ya umeme kwa wananchi vijijini na kufuata maagizo yote yanayotolewa na viongozi ngazi za juu pamoja na kuziainisha changamoto zinazokwamisha miradi hiyo kwa wakati, ili Serikali iweze kuzitatua na wananchi wote wanufaike na umeme.

Nao wanufaika wa umeme huo waliishukuru

Serikali ya Awamu ya Tano, kupitia TANESCO kwa kuweza kuleta mwanga katika kijiji hicho na kuondokana na hali ya giza iliyokuwepo awali.

Timu hiyo inayoongozwa na Mhandisi Luoga inawajumuisha pia Naibu Mkurugenzi TANESCO, Mhandisi Raymond Seya, Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Jones Olotu, Afisa kutoka Wizara ya Nishati anayesimamia miradi ya Umeme Vijijini, Mhandisi Dauson Kamaka na Mafafisa wanaosimamia Mradi huo kutoka TANESCO na REA.

Ikiwa katika Mkoa wa Arusha, pamoja na kuwasha umeme Lendikinya, Timu hiyo pia ilikagua usambazaji wa umeme katika mitaa ya Muriyet na Terrat.



Baadhi ya wakazi wa kijiji cha Lendikinya wakifuatilia hotuba ya Mgeni Rasmi, Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Robert Syantemi (hayupo pichani), wakati wa hafla ya uwashwaji umeme katika kijiji hicho, Septemba 11, 2020.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Iddi Hassan Kimanta (katikati) akiwa katika kikao na Timu Maalum ya Serikali iliyoungwa na Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani) kufuatilia utekelezaji wa miradi ya umeme mijini na vijijini.

JNHPP KUZUIA GESI JOTO TANI MILIONI SABA KWA MWAKA



Timu ya Kitaifa ya Wataalamu inayofuatilia hali ya uhifadhi wa rasilimali maji ya Bonde la Mto Rufiji, wakiwa katika picha ya pamoja, wakati wa ziara ya kutembelea na kuona maendeleo ya ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere (Julius Nyerere Hydro Power Project - JNHPP), Septemba 19, 2020.

Zuena Msuya - Pwani

Timu ya Kitaifa ya Wataalamu inayofuatilia hali ya uhifadhi wa rasilimali maji katika Bonde la Mto Rufiji, imesema kuwa, mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Julius

Nyerere (Julius Nyerere Hydro Power Project - JNHPP), ndiyo mradi pekee Afrika utakozuia gesi joto takribani tani milioni 7.6 kwa mwaka katika uso wa dunia

Walieleza hayo Septemba 19, 2020 walipofanya ziara na

kujionea maendeleo ya ujenzi wa mradi huo unaotekelezwa wilayani Rufiji, Mkoa wa Pwani.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Mkuu wa Idara ya Mazingira kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dkt. Richard Muyungi,

alisema kuwa, uwepo wa mradi huo utaisaidia dunia kupambana na uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi ambao umekuwa ukitokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo vya uzalishaji wa nishati ya umeme kwa kutumia joto ardhini pamoja na gesi.

“Mradi huu una faida za ziada tofauti na zile zinazoelezwa. Tumefanya utafiti na kubaini kuwa, endapo mradi huu usingejengwa, basi tungezalisha umeme kwa kutumia vyanzo vingine kama gesi na joto ardhini ambavyo vingezalisha gesi joto takribani tani milioni 7.6 kwa mwaka, ambazo zingechafua mazingira na uso wa dunia. Lakini kwa kutumia maji, hatutazalisha gesi hizo,” alifafanua Dkt. Muyungi.

Akieleza zaidi, alisema kuwa, Bwawa hilo litakuwa na maji ya uhakika yatakatumiwa pia na wanyama na hivyo kuwawezesha kuendelea kuishi katika eneo hilo kwa muda mrefu.

Aidha, Dkt. Muyungi aliongeza kuwa, baada ya eneo hilo kutangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa, kumeongeza ulinzi wa

INAENDELEA UK.

16



Timu ya Kitaifa ya Wataalamu inayofuatilia hali ya uhifadhi wa rasilimali ya maji ya Bonde la Mto Rufiji, wakiwa ndani ya handaki la kuchepusha maji ya mto wakati wa ziara yao waliyoifanya Septemba 19, 2020 kujionea maendeleo ya ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (Julius Nyerere Hydro Power Project - JNHPP)

INATOKA UK.

15

wanyama, mimea pamoja na uasilia wake na endapo mradi huo usingefanywa na eneo hilo kutokuwa hifadhi ya taifa, viumbe wa eneo hilo wanguweza kudhuriwa na eneo husika kupoteza uhalisia wake kwa sababu ya ulinzi kuwa haffu pamoja na uendeshaji wa shughuli mbalimbali za kibinadamu.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mradi wa JNHPP kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Yusuph Msembele, alisema kuwa lengo la ziara hiyo ilikuwa kuwaonyesha wataalamu wa timu hiyo maendeleo ya mradi ili wapate hamasa katika kusimamia matumizi bora ya rasilimali maji katika Bonde la Mto Rufiji kwa kuwa taasisi zao ndizo zenye dhamana ya kutekeleza usimamizi wa sheria za uhifadhi.

Hivyo, Mhandisi Msembele, aliwasisitiza wajumbe wa Timu hiyo kuendelea kuwa mabalozi wazuri katika kuhamasisha wananchi kuzingatia matumizi bora na sahihi ya maji katika ukanda wa vyanzo vya maji ya Bonde la Mto Rufiji.

Naye, Mhandisi Mkazi na Mshauri wa mradi huo,

JNHPP KUZUIA GESI JOTO TANI MILIONI SABA KWA MWAKA



Timu ya Kitaifa ya Wataalamu inayofuatilia hali ya uhifadhi wa rasilimali ya maji ya Bonde la Mto Rufiji, wakioneshwa eneo litakapojengwa jengo la kuendesha mitambo. Timu hiyo ilifanya ziara ya kutembelea na kuona maendeleo ya ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (Julius Nyerere Hydro Power Project - JNHPP), Septemba 19, 2020.

Mushubila Kamuhabwa, aliieleza timu hiyo kuwa, ujenzi wake unaendelea vizuri na uko katika hatua nzuri za utekelezaji.

Timu hiyo ya wataalamu inaundwa na Wajumbe Kutoka ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za

Mitaa (TAMISEMI), Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Uratibu, Wizara ya Nishati, na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Nyingine ni Wizara ya Kilimo, Wizara ya

Maji, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Bonde la Mto Rufiji.



Kazi ya kusuka nondo ikiendelea ndani ya handaki la kuchepusha maji katika Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (Julius Nyerere Hydro Power Project - JNHPP). Taswira hii ilichukuliwa Septemba 19, 2020 wakati wa ziara ya Timu ya Kitaifa ya Wataalamu inayofuatilia hali ya uhifadhi wa rasilimali ya maji ya Bonde la Mto Rufiji.



Vijana wakibeba nondo ndani ya handaki la kuchepusha maji ya mto wakati wa ujenzi wa ukuta wa kuzuia maji ya bwawa, katika Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (Julius Nyerere Hydro Power Project - JNHPP). Taswira hii ilichukuliwa Septemba 19, 2020 wakati wa ziara ya Timu ya Kitaifa ya Wataalamu inayofuatilia hali ya uhifadhi wa rasilimali ya maji ya Bonde la Mto Rufiji.

MWANGA WANUFAIKA NA MIRADI YA UMEME VIJIJINI



Mkuu wa Wilaya ya Mwangi, Thomas Apson akikata utepe kabla ya kuwasha umeme katika kijiji cha Kiverenge, wakati wa ziara ya Timu maalum ya Serikali iliyoungwa kufuatilia utekezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini mkoani Kilimanjaro, Septemba 3, 2020.

Na Mwandishi wetu - Kilimanjaro

Wilaya ya Mwangi mkoani Kilimanjaro imeendelea kunufaika na miradi ya umeme

vijijini baada ya kijiji cha Vuchamangofi, Kata ya Mwaniko na kijiji cha Kiverenge, Kata ya Mwangi kuwashiwa umeme na Timu maalumu ya Serikali iliyoungwa hivi karibuni kwa lengo la kufuatilia utekezaji wa miradi ya umeme vijijini

mkoani humo.

Timu hiyo inayoongozwa na Kamishna Msaidizi wa Umeme, Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga, iliundwa na Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani wakati wa ziara yake kukagua maendeleo ya usambazaji umeme mkoani Kilimanjaro.

Akizungumza wakati wa ziara ya Timu hiyo wilayani Mwangi, Septemba 3, 2020, Mhandisi Luoga alimweleza Mkuu wa Wilaya hiyo, Thomas Apson kuwa Timu yake imefanikiwa kutatua changamoto zinazowakabili wakandarasi wanaotekeleza mradi wa umeme vijijini wilayani humo.

Aliongeza kuwa, Timu hiyo itawezesha uwashaji wa umeme katika vijiji vyote vilivyosalia ifikapo mwishoni mwa mwezi Septemba, 2020.

"Tumefanikiwa kutatua changamoto zinazowakabili wakandarasi ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa vifaa mbalimbali

zikiwemo nguzo, nyaya, mita na transfoma, hivyo wakandarasi wote watakamilisha kazi kwa wakati."

Awali, akiwasha umeme katika Kijiji cha Kiverenge, Mkuu wa Wilaya ya Mwangi, Thomas Apson aliipongeza Timu hiyo kwa kufanyia kazi changamoto za wakandarasi na kuwezesha uwashaji wa umeme katika vijiji vya Wilaya hiyo.

Alisema kuwa Wilaya ya Mwangi ina jumla ya vijiji 72 ambapo 68 kati yake, tayari vina umeme. Aidha, alisema Timu hiyo imemhakikishia kuwa vijiji vinne vilivyobaki vitapata umeme kabla ya Septemba 15, 2020.

"Naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi hii nzuri ya kufikisha umeme katika vijiji vyote nchini. Nawapongeza sana wataalam kwa kufika hapa Kiverenge na kutatua changamoto zilizopo," alisema Mkuu huyo wa Wilaya.

Katika ziara hiyo, Timu ilifanya vikao na viongozi mbalimbali wa serikali akiwemo Mkuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Watendaji wa Kata na Wenyeviti wa Vijiji ili kusikiliza changamoto za wananchi katika utekezaji wa Mradi.



Mkuu wa Wilaya ya Mwangi, Thomas Apson akizungumza na wananchi, wakati wa ziara ya Timu maalum ya Serikali iliyoungwa kufuatilia utekezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini Mkoani Kilimanjaro, Septemba 3, 2020.



Mafundi wa Mkandarasi wa Kampuni ya U&R wakifunga Transfoma katika Kijiji cha Vuchamangofi wilayani Mwangi, ikiwa ni maandalizi ya uwashaji wa umeme, wakati wa ziara ya Timu maalum ya Serikali iliyoungwa kufuatilia utekezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini Mkoani Kilimanjaro, Septemba 3, 2020.

REA YAZINUFAISHA SHULE, MISIKITI NA MAKANISA KILIMANJARO

Na Mwandishi wetu - Kilimanjaro

Timu maalum ya Serikali iliyoundwa kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini mkoani Kilimanjaro, imewasha umeme katika Taasisi zinazotoa huduma kwa jamii zikiwemo shule za msingi, sekondari, misikiti na makanisa mkoani humo hivyo kuleta neema kwa wananchi.

Timu hiyo inayojumuisha wataalamu kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zake zinazohusika na umeme, ikiongozwa na Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga iliundwa na Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani wakati wa ziara yake kukagua maendeleo ya usambazaji umeme katika Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro hivi karibuni.

Akielezea lengo la ziara ya Timu hiyo iliyofanikisha kuwashwa umeme kwa Taasisi hizo za umma, Mhandisi Luoga alisema kuwa ilijikita katika kutatua changamoto zinazowakabili wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini katika Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha ili kuhakikisha wananchi wananufaika na nishati hiyo.

Alisema, ziara ilifanyika kwa siku nane katika Wilaya za Same, Mwanaga, Rombo, Moshi, Siha na Hai kuanzia Septemba 1, 2020.

"Tumefanikiwa kuwasha umeme katika shule, makanisa, misikiti, zahanati, vituo vya afya pamoja na ofisi mbalimbali za serikali," alifanua Mhandisi Luoga.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Hai, Upendo Wella akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Roo kabla ya kuwasha rasmi umeme, wakati wa ziara ya Timu maalum ya Serikali iliyoundwa kufuatilia utekelezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini Mkoani Kilimanjaro, Septemba 7, 2020.

Alieleza baadhi ya changamoto ambazo Timu yake ilizibaini na kuzitatua, kuwa ni pamoja na uwepo wa nguzo zilizosimikwa pasipo kuvutiwa nyaya na kuwepo kwa orodha ndefu ya wateja wanaosubiri kuunganishiwa umeme.

Katika ziara hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Dkt. Othman Kihamia, aliwasha umeme katika kanisa la TAG na Mhandisi Luoga

aliwasha umeme katika shule ya msingi ya Nasea iliyopo katika Kijiji cha Nasea Wilayani Rombo.

Awali, akiwasha umeme katika Shule ya Sekondari ya Rombo iliyopo Hai, Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Upendo Wella akimwakilisha Mkuu wa Wilaya, aliipongeza Wizara ya Nishati kwa kazi kubwa na nzuri inayoifanya kufikisha umeme katika

vijiji na Taasisi za Umma.

"Umeme huu ulete mabadiliko ya kiuchumi na kijamii pamoja na kuwezesha wanafunzi kufanya mafunzi kwa vitendo na hivyo kuongeza ufaulu hapa shuleni. Naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano na Timu hii ya Serikali kwa kazi hii nzuri," alisema.

Aidha, akiwasha umeme katika kitongoji cha Kideko, kilichopo katika kijiji cha Majengo, Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu aliipongeza Wizara kwa kazi nzuri ya kupeleka umeme katika vijiji vyote nchini vikiwemo vya Wilaya yake.

"Wilaya ya Siha ina jumla ya vijiji 60 na hadi kufikia leo tayari vijiji 58 vina umeme na nimejulishwa na Kamishna kuwa vijiji viwili vilivyobaki vitapata umeme kabla ya tarehe 15/9/2020. Naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano na Wizara ya Nishati kwa kazi hii nzuri."



Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu akizungumza na wananchi wa kijiji cha Roselini, kitongoji cha Mjimwema, wakati wa ziara ya Timu maalum ya Serikali iliyoundwa kufuatilia utekelezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini, Mkoani Kilimanjaro Septemba 7, 2020.

SERIKALI YAHIMIZA KUKAMILISHWA KWA WAKATI KITUO CHA KUPOZA UMEME NYAKANAZI



Kamishna Msaidizi wa Umeme kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga (wa pili-kushoto) na Ujumbe wake, wakikagua ramani ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Nyakanazi, walipozuru kituo hicho Septemba 30, 2020 kujionea maendeleo yake.

Veronica Simba – Ngara

Serikali imehimiza kukamilishwa kwa wakati, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Nyakanazi ili pamoja na manufaa mengine, kiwaondolee wananchi wa Mkoa wa Kagera, adha ya kutokupata umeme wa kutosha.

Kamishna Msaidizi wa Umeme kutoka Wizara

ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga alitoa maelekezo hayo, Septemba 30, 2020 kwa Mkandarasi anayetekeleza Mradi huo, Kampuni ya L & T Construction kutoka India.

Akiwa amefuatana na Meneja Mwandamizi wa Uwekezaji kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mhandisi Costa Rubagumya pamoja na Mhandisi Mkuu wa



Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo ikikagua maendeleo ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Nyakanazi, wakiwa katika ziara ya kazi, Septemba 30, 2020.

Nishati kutoka Wizarani, Salum Inegeja, alimtaja Mkandarasi kutumia mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kukamilisha Mradi huo ifikapo Februari 2021, kama ilivyo kwenye Mkataba.

Mhandisi Luoga alibainisha kuwa kituo hicho kinategemewa na miradi mingine kadhaa ya

umeme na kwamba pasipo ujenzi wake kukamilika, miradi hiyo pia haitaweza kuwanufaisha wananchi.

“Mathalani, ili rradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Rusumo hadi hapa

INAENDELEA UK.

20



Meneja wa Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme (kilovoti 220) kutoka Rusumo hadi Nyakanazi Mhandisi Paschal Kibasa (kushoto) akionesha eneo kutakapojengwa kituo cha kupoza umeme Benaco, wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera kwa Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo. Timu hiyo ilikuwa katika ziara ya kazi Septemba 30, 2020.



Kazi ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Nyakanazi ikiendelea. Taswira hii ilinaswa wakati wa ziara ya Timu ya Serikali inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo, kukagua maendeleo ya utekelezaji wake, Septemba 30, 2020. Kituo hicho kinatarajiwa kukamilika Februari, 2021.

SERIKALI YAHIMIZA KUKAMILISHWA KWA WAKATI KITUO CHA KUPOZA UMEME NYAKANAZI

INATOKA UK.

19

Nyakanazi, umbali wa kilomita 94, uweze kufanya kazi, unategemea Mradi huu wa kituo cha kupoza umeme ukamilike.”

“Pia, unahusisha mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Geita mpaka hapa Nyakanazi, umbali wa kilomita 54,” alisema.

Akifafanua zaidi kuhusu manufaa ya kituo hicho, alisema kikamilika kitasaidia kuboresha hali ya upatikanaji umeme katika mikoa ya Geita, Kigoma na Kagera ambayo itaingizwa katika gridi ya Taifa kama alivyoagiza Rais John Pombe Magufuli.

Alisema kuwa tafsiri ya uwepo wa umeme wa uhakika inamaanisha shughuli za kijamii na kiuchumi zitaboreshwa

hivyo Pato la Taifa litaongezeka.

Alieleza manufaa mengine ya kukamilika kwa kituo hicho kuwa ni kuwezesha biashara ya umeme baina ya Tanzania na nchi jirani zikiwemo Rwanda na Burundi kwani kituo hicho kitaunganishwa na kituo cha Rusumo, ambacho Mradi wake wa kuzalisha umeme unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya nchi hizo tatu.

Kuhusu mbinu ambazo alishauri Mkandarasi azitumie kukamilisha kazi kwa wakati, Mhandisi Luoga alizitaja kuwa ni pamoja na kuongeza idadi ya wafanyakazi pamoja na kuongeza muda wa kufanya kazi.

Pamoja na kutoa maelekezo hayo, Mhandisi Luoga alikiri kuwa yeyé pamoja na



Kamishna Msaidizi wa Umeme kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga (katikati), akisikiliza maelezo kutoka kwa Meneja wa Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme (kilovoti 220) kutoka Rusumo hadi Nyakanazi Mhandisi Paschal Kibasa (kulia), wakati wa ziara ya kazi kukagua maendeleo ya utekezaji wa mradi huo. Kushoto ni Mhandisi Mkuu kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Salum Inegeja.



Kutoka kushoto ni Meneja Mwandamizi wa Uwekezaji kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mhandisi Costa Rubagumya, Afisa Mwandamizi, Jamii, Maendeleo na Uhamaji Makazi kutoka NELSAP, Gaspar Mashingia pamoja na Mhandisi Mkuu wa Nishati kutoka Wizara ya Nishati, Salum Inegeja wakiwa katika ziara ya Timu ya Serikali (wengine hawapo pichani) kukagua maendeleo ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme (kilovoti 220) kutoka Rusumo hadi Nyakanazi, Septemba 30, 2020.

wenzake alioambatana nao wameridhishwa na hatua iliyofikiwa katika utekezaji wa Mradi huo hivyo akampongeza Mkandarasi husika kwa utendaji mzuri.

Kwa upande wake, Mkandarasi huyo alimhakikishia Mhandisi Luoga na Ujumbe wake kuwa kampuni yake imejipanga kukamilisha kazi hiyo kwa wakati na viwango stahiki ili kutunza rekodi yao ya utendaji kazi mzuri inayotambulika duniani kote.

Awali, Timu hiyo ya wataalamu kutoka serikalini ilikagua maendeleo ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme (kilovoti 220) kutoka Rusumo hadi Nyakanazi, wakiwa wameambatana na Meneja wa Mradi husika,

Mhandisi Paschal Kibasa ambapo walishuhudia kazi za awali za utekezaji zikiendelea kwa kasi.

Aidha, Timu hiyo ilikagua eneo kutakapojengwa kituo cha kupoza umeme Benaco ambacho kitapeleka umeme Kyaka hivyo kuwezesha kuunganisha Mkoa wote wa Kagera kwenye Gridi ya Taifa.

Timu hiyo ya Serikali imekamilisha ziara yake ya siku tatu wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera, ambayo ilihusisha kukagua miradi mbalimbali ya kijamii inayotekelezwa kupitia Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera (megawati 80), ukizijumuisha nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi.



Kamishna Msaidizi wa Umeme kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga (katikati), akisikiliza maelezo kutoka kwa wataalamu wa kampuni ya ukandarasi ya JV WSP & GOPA INTEC, inayotekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme (kilovoti 220) kutoka Rusumo hadi Nyakanazi, akiwa katika ziara ya kazi, Septemba 30, 2020.



Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo ikikagua maendeleo ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme (kilovoti 220) kutoka Rusumo hadi Nyakanazi. Timu hiyo ilikuwa katika ziara ya kazi, Septemba 30, 2020.

Timu ya Serikali kutoka Tanzania inayosimamia Mradi wa Umeme wa Rusumo, wakiwa katika picha ya pamoja na Menejimenti na wafanyakazi wa Kampuni ya Ukandarasi L & T Construction inayotekeleza Mradi wa Ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Nyakanazi. Timu hiyo ilikuwa katika ziara ya kazi, Septemba 30, 2020.



KIJIJI CHA NASURO WILAYANI SAME CHAWASHIWA UMEME

Na Mwandishi wetu - Kilimanjaro

Kijiji cha Nasuro kilichoko wilayani Same, Mkoa wa Kilimanjaro, kimewashiwa umeme rasmi Septemba 2, 2020 kupitia Mradi wa Umeme Vijijini unaoendelea kutekelezwa nchini kote.

Akizungumza na wananchi wa kijiji hicho, muda mfupi kabla ya kuwasha umeme, Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule aliipongeza Wizara ya Nishati kwa kazi inayoifanya ya kuhakikisha nishati hiyo muhimu, inawafikia wananchi wote nchini.

Alisema kuwa Wilaya ya Same ina vijiji 100 ambapo kati yake, 91 vimekwishapata umeme na kwamba vijiji tisa vilivyobaki vitapata umeme kabla ya Septemba 15, 2020.

Kuwashwa kwa umeme katika kijiji hicho



Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule akikata utepe kabla ya kuwasha umeme katika kijiji cha Nasuro wilayani humo, wakati wa ziara ya Timu maalum ya Serikali iliyoungwa kufuatilia utekelezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini, Septemba 2, 2020 mkoani Kilimanjaro.

ni kufuatia ziara ya Timu maalum ya Serikali iliyoungwa kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zake zinazohusika na umeme, kufuatilia utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini mkoani Kilimanjaro. Timu hiyo

inayoongozwa na Kamishna Msaidizi wa Umeme, Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga iliundwa na Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani, wakati wa ziara yake kukagua maendeleo ya usambazaji umeme

mkoani humo hivi karibuni.

Mhandisi Luoga alisema timu yake imewezesha kuwashwa kwa umeme katika maeneo mbalimbali, kikiwemo kijiji hicho cha Nasuro baada ya kutatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili wakandarasi wanaotekeleza miradi husika katika Mkoa wa Kilimanjaro na Arusha, ambazo ni Kampuni za State Grid, Octopus na Njarita.

"Tumetatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili wakandarasi ili kuharakisha utekelezaji wa Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza na ule wa Awamu ya Pili ambao utekelezaji wake unasuasua ili nao uweze kukamilika kwa wakati na kuwasha umeme vijiji vyote ifikapo mwishoni mwa mwezi huu wa Septemba," alifafanua.

Alieleza baadhi ya changamoto zinazowakabili wakandarasi hao, kuwa ni pamoja na uwepo wa nguzo zilizosimikwa pasipo kuvutiwa nyaya na kuwepo kwa orodha ndefu ya wateja wanaosubiri kuunganishiwa umeme.

Kuhusu changamoto ya upatikanaji wa vifaa vya wakandarasi hao, Mhandisi Luoga alisema kuwa tayari wakandarasi hao wana vifaa vyote vinavyotakiwa kutekeleza mradi zikiwemo nyaya, nguzo, mita na transfoma.

Aidha, alieleza kuwa kazi zilizofanywa na timu hiyo ni kufanya vikao na viongozi mbalimbali wa serikali akiwemo Mkuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Watendaji wa Kata na Wenyeviti wa Vijiji ili kusikiliza changamoto za wananchi katika utekelezaji wa Mradi.



Kamishna Msaidizi wa Umeme kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga, akitoa maelezo ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini katika Wilaya ya Same, wakati wa ziara ya Timu maalum ya Serikali iliyoungwa kufuatilia utekelezaji wa mradi huo, Mkoani Kilimanjaro.



Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule akizungumza na wananchi wakati wa ziara ya Timu maalum ya Serikali iliyoungwa kufuatilia utekelezaji wa mradi wa usambazaji umeme vijijini katika Mkoani Kilimanjaro, Septemba 2, 2020.

RAIS AMEWAAMINI WAZALENDO KUTEKELEZA JNHPP – NAIBU KATIBU MKUU MASANJA



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, akizungumza na Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara husika (kulia) pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (kushoto), wakati Ujumbe huo ulipozuru Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji mkoani Pwani ili kujionea maendeleo yake, Oktoba 03, 2020.



Veronica Simba – Rufiji

Naiibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, amempongeza Rais John Pombe Magufuli kwa kuwaamini wazalendo katika kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP).

Alitoa pongezi hizo Oktoba 3, 2020 wakati akizungumza na Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REB), waliotembelea Mradi huo unaotekelezwa wilayani Rufiji, Mkoa wa Pwani, ili kujionea maendeleo yake.

Mhandisi Masanja alisema kuwa hatua ya Mheshimiwa Rais kuwaamini wataalamu wazalendo kusimamia

usanifu wa awali, hatua za manunuzi na hata usimamizi wa utekelezaji wa mradi wenyewe, pasipo kushirikisha wataalamu wa kigeni ni ushahidi kuwa Tanzania ina hazina ya wataalamu mahiri.

“Kupitia Mradi huu, tumeudhirishia ulimwengu kuwa Tanzania ina wataalamu mahiri na kwamba sisi wenyewe tunaweza kusimamia miradi yetu.”

Akifafanua, alieleza kuwa Serikali iliamua kuwatumia wataalamu kutoka TANROADS (TANROADS Engineering Consulting Unit - TECU) kama Mshauri Mwelekezi wa Mradi na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kama wawakilishi wa Serikali katika kusimamia Mradi husika ili kuhakikisha

Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REB), wakikagua miundombinu mbalimbali inayoendelea kujengwa katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji mkoani Pwani. Ujumbe huo ulitembelea Mradi husika, Oktoba 03, 2020 ili kujionea maendeleo yake.

RAIS AMEWAAMINI WAZALENDO KUTEKELEZA JNHPP – NAIBU KATIBU MKUU MASANJA

INATOKA UK.

23

Mkandarasi anatekeleza kazi zote kwa mujibu wa Mkataba.

Aidha, aliongeza kuwa, jambo la kujivunia zaidi ni kuwa Mradi huo unatekelezwa na fedha za Serikali kwa asilimia 100, hivyo akawataka Watanzania kujivunia Mradi huo kwani nchi inaumiliki kikamilifu.

Awali, akitoa wasilisho la Mradi kwa Ujumbe husika, Mhandisi Mkazi wa Mradi huo, Mushubila Kamuhabwa, alisema kuwa katika hatua ya ujenzi inayoendelea sasa, Mradi umewezesha uzalendo na mshikamano wa hali ya juu kwa vijana wa kitanzania wanaofanya kazi za ujenzi.

“Ni kama wakati ule vijana walipokuwa wakishirikiki mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa. Utawakuta vijana hawa wakiimba nyimbo za kizalendo wakati wanafanya kazi na pia wakishirikiana kwa kila jambo, hali inayoonesha wazi wanajisikia fahari kuwa sehemu ya utekelezaji wa Mradi huu.”

Vilevile, Mhandisi Kamuhabwa alibainisha kuwa miongoni mwa waajiriwa 5,500 wa Mradi waliopo sasa, Watanzania ni 4,900 ambao ni takribani asilimia 90 wa waajiriwa wote, jambo ambalo linadhihirisha dhamira ya Serikali kuhakikisha Watanzania wanapewa kipaumbele katika kila sekta ya Mradi huo.

Aidha, alibainisha faida nyingine ambazo zimekwishaanza kupatikana katika hatua hii ya awali ya utekelezaji wa Mradi kuwa ni pamoja na matumizi ya rasilimali

za ndani ya nchi kama vile nondo, saruji, vyakula, ulinzi na nyinginezo.

Kuhusu faida zitakazopatikana baada ya kukamilika kwa Mradi, alisema pamoja na kuzalisha umeme mwingi utakaokuwa na bei nafuu, Mradi huo pia utakuza sekta za utalii, kilimo, uvuvi wa samaki pamoja na kuboresha mazingira kutokana na kupungua kwa ukataji miti kwa matumizi ya mkaa na kuni.

Alitaja faida nyingine kuwa ni kudhibiti mafuriko kwa kudhibiti maji ya Mto Rufiji ambayo awali yalikuwa yakileta majanga ya kuuu watu na kuharibu mali zao.

Akizungumza kwa niaba ya Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini, Mwenyekiti wake, Wakili Julius Kalolo alipongeza kazi inayofanyika ambapo alisema yeyé na wenzake wameridhishwa na kasi pamoja na viwango katika utekelezaji huo wa Mradi.

Aliongeza kuwa pindi Mradi huo utakapokamilika utaongeza nguvu zaidi kwa Wakala huo kufikisha umeme kwa kila kaya, ikizingatiwa kuwa tayari taasisi hiyo imeanza utekelezaji wa kupeleka umeme katika kila kitongoji nchini.

Naye Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu kutoka Wizara ya Nishati, Edward Ishengoma alisema kuwa Wizara iliona umuhimu wa kuandaa ziara hiyo kwa ajili ya Wajumbe wa Menejimenti yake, ili kuwawezesha kujionea kwa macho kinachofanyika ikizingatiwa kuwa ndiyo Wizara Mama inayohusika na Mradi huo.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (katikati), akiwa na Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REB), wakati Ujumbe huo ulipotembelea Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji mkoani Pwani, Oktoba 03, 2020 ili kujionea maendeleo yake.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REB) baada ya Ujumbe huo kuhitimisha ziara yake katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji mkoani Pwani, Oktoba 03, 2020, iliyolenga kujionea maendeleo yake.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (Rural Energy Board - REB), Wakili Julius Kalolo, akizungumza neno, wakati Bodi hiyo (kushoto) na Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati (kulia), walipotembelea Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji, mkoani Pwani, Oktoba 03, 2020 ili kujionea maendeleo yake. Wa kwanza kushoto ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja.



Mhandisi Mkazi wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Mushubila Kamuhabwa, akitoa wasilisho la Mradi huo kwa Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati (kulia) pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (kushoto), walipozuru Mradi huo, Rufiji mkoani Pwani, Oktoba 03, 2020 ili kujionea maendeleo yake.



Ujenzi wa miundombinu mbalimbali ukiendelea katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji, mkoani Pwani. Taswira hii ilichukuliwa Oktoba 03, 2020 wakati Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (hawapo pichani), walipozuru Mradi huo ili kujionea maendeleo yake.



Baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kutembelea Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji mkoani Pwani, Oktoba 03, 2020 ili kujionea maendeleo yake.

MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WAJUMBE WA MENEJIMENTI YA WIZARA YA NISHATI PAMOJA NA BODI YA WAKURUGENZI WA WAKALA WA NISHATI VIJIJINI, WALIPOTEMBELEA MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE, RUFJI MKOANI PWANI, KUJIONEA MAENDELEO YAKE, OKTOBA 03, 2020



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (wa sita kutoka kushoto), akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati baada ya Ujumbe huo kuhitimisha ziara yake katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji mkoani Pwani, Oktoba 03, 2020, iliyolenga kujionea maendeleo yake.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (wa tano kutoka kushoto), akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REB) baada ya Ujumbe huo kuhitimisha ziara yake katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji mkoani Pwani, Oktoba 03, 2020, iliyolenga kujionea maendeleo yake.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REB) pamoja na Menejimenti ya Wakala huo, baada ya Ujumbe huo kuhitimisha ziara yake katika Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere, Rufiji mkoani Pwani, Oktoba 03, 2020, iliyolenga kujionea maendeleo yake.

Matukio mbalimbali wakati Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati pamoja na Wakurugenzi wa Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REB) walipotembelea Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) kujionea maendeleo yake, Oktoba 03, 2020.

MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WAJUMBE WA MENEJIMENTI YA WIZARA YA NISHATI PAMOJA NA BODI YA WAKURUGENZI WA WAKALA WA NISHATI VIJIJINI, WALIPOTEMBELEA MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE, RUFUJI MKOANI PWANI, KUJIONEA MAENDELEO YAKE, OKTOBA 03, 2020



Matukio mbalimbali wakati Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati pamoja na Wakurugenzi wa Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REB) walipotembelea Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) kujionea maendeleo yake, Oktoba 03, 2020.

JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



Fika Ofisi ya Mawasiliano,
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
Nukushi +255-26-2320148

 www.nishati.go.tz

 [Wizara ya Nishati](#)

 [@Nishati2017](#)

 [wizara_ya_nishati_tanzania](#)

 [Wizara ya Nishati](#)